# <u>KUJUTIA DHAMBI</u>

# <u>MAANDIKO: LUK. 18: 9-14 na Luk. 16: 19 - 31</u>

1. **<u>UTANGULIZI</u>**

**Kuna vipindi viwili alivyo navyo mwanadamu vya kujutia dhambi zake anazozijua kwamba amezifanya katika maisha yake.**

A. **<u>Kujutia dhambi zako zote wakati unapokuwa hai kimwili na kiroho,</u>** (kutubu) na majuto (toba) ya namna hii ndiyo ambayo mara zote yanamletea faida ya kupata wokovu kama ilivyotokea kwa huyu mtoza ushuru pamoja na baraka nyingine tele tele. (toba ya hiari na siyo kungoja kubembelezwa, ni toba inayotoka ndani ya moyo kabisa.

- **<u>La kujua kwa kina kuhusiana na mtu anayejutia kabisa dhambi zake mbele za Mungu wakati akiwa hai ni kwamba;toba ya kweli ina faida nyingi zifuatazo</u>:-**

i. **Toba yetu ya kweli ndiyo njia pekee na maalumu sana inayotuunganisha na Mungu na kutufanya tuweze kukaa naye pamoja tena na hata yeye Mungu kuwa radhi kusikia maombi yetu na kutujibu. *Yoh. 9:30-31, Efes. 2:11-19 (Yoh. 1:12) ( Soma pia Luk. 15: 10 – 24 (toba ya mwana mpotevu au toba ya Mfalme wa Ninawi na watu wake – Yona 3: 1 – 10.***

ii. **Pale tunapotubu dhambi zetu na kuzijutia kabisa wakati tukiwa hai Yesu Kristo anasimama mbele za Mungu Baba yake na kututetea kwa umakini wa hali ya juu sana jambo ambalo linamfanya Mungu Baba akumbuke kazi kubwa aliyoifanya Yesu Kristo pale msalabani na kutufutia (kutuondolea) hukumu zote (mabaya yote ambayo tungeyapata kutokana na dhambi tulizofanya yanafutwa)**

iii. **Wakati mwingine kwa mujibu wa neno la Mungu. Toba ya kweli (kujutia dhambi) hufungulia mlango haraka sana wa uponyaji wa magonjwa ambayo yalikuwa yanamtesa mtu kwa muda mrefu na kufanya mtu aliyekuwa amechakaa kwa sababu ya magonjwa yaliyosababishwa na maisha yake ya dhambi ang'arishwe. *Mark.5:25-34,Zab.103:1-5,1Wafal. 21:17-29.***

iv. **Lakini pia toba ya kweli wakati ukiwa hai ndiyo inayokuongezea siku za kuishi na kuifukuzia mbali roho ya mauti iliyokuwa inakukabili saa zote.** ***Yoh.8:1-11.***

v. **Lakini lililo kubwa zaidi kulielewa ni hili kwamba "toba ya kweli (kujutia dhambi) wakati ukiwa hai ndiyo ufunguo wa kuanza kupokea baraka halisi kutoka kwa Mungu ikiwa ni pamoja na Mungu kuachilia nguvu zake zianze kukuendesha katika maisha yako"** ***Luk. 19:1-10, Mdo.9:1-9, 17-18***

***Mfano*****: Toba ya Zakayo akiwa hai.** Majuto yake ya kujutia dhambi zake zote alizofanya pamoja na kuweka kando cheo chake na heshima yake yote aliyokuwa nayo kwa ajili ya kutaka kumwona Yesu Kristo ndivyo vilivyomfanya Yesu Kristo naye akubali kushinda nyumbani kwa Zakayo na kula naye na kuwa na mazungumzo marefu. **Hii ilikuwa ni heshima ya hali ya juu sana na cheo cha juu sana alichopewa Zakayo na Yesu Kristo kwani kuna baadhi ya wanafunzi wake ambao hatuna hakika kama Yesu alifika nyumbani kwao na kukaa nao hata saa moja na wakampikia na kula nao**: Lakini kwa Zakayo Yesu Kristo akashinda siku nzima!! Heshima kubwa mno na urafiki wa hali ya juu mno!! Aliopewa Zakayo mkuu wa watonza ushuru; yote hii ni kwa sababu Zakayo alitubu hadharani bila kuogopa watu watamwonaje; **Zakayo hakulazimishwa na mtu kutubu dhambi zake bali alitubu kwa hiari yake: Kwa hakika Zakayo alionyesha unyenyekevu wa hali ya juu mno kwa Bwana Yesu (Mkuu wa Watoza ushuru kwenda kupanda juu ya Mkuyu kwa kusudi tu la kutaka kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, akaweka pembeni cheo chake chote na utajiri wake wote na kupanda juu ya Mkuyu na kitambi chake; kweli Yesu alimwona Zakayo alivyomtamani kutoka ndani ya moyo wake!!!** Zakayo akapokea baraka toka kwa Bwana hata kuzidi wale waliomshughudia habari za Yesu; na wakati mwingine hata kuzidi baadhi ya Wanafunzi wake ambao Yesu alikuwa anazunguka nao kila mahali.

**B. Kujutia dhambi zako baada ya kufa kimwili au kiroho; wakati unakabiliwa na hukumu (hii ni toba na majuto ya dhambi wakati tayari UMECHELEWA.** ***Luk. 16: 19 – 31.*** **Math.27: 3 – 5.**

**La muhimu sana kujua katika toba hii baada ya kufa kimwili au kiroho ni kwamba kamwe kamwe haina uwezo wa kubadilisha chochote tena (haiwezi kubadilisha hukukmu yako ambayo inakukabili. Mhub. *11:3, Ebr.9:27,***

- **Yuda alitubu wakati amechelewa kama Akani naye. Math. 27: 3 – 5, Yosh. 7: 1, 19-21**

- Kusubiri ufe au uugue sana kiasi cha kufa ndipo uanze kujutia dhambi zako/ zangu au ubembelezwe sana mara zote hakutamfanya mhusika apate manufaa ya aina yeyote!! Hata kama utaongozwa sala ya toba ukiwa kitandani hoi bini taabani na baada ya sala hiyo ya toba kama ya kulazimishwa unakufa; umenufaika nini, hata waliokuongoza sala hiyo hawana hakika kama umepokelewa na Bwana (inabaki kuwa siri ya Bwana mpaka siku tutakapofika huko juu!! Hata mhalifu mkubwa pale msalabani hakulazimishwa kutubu dhambi zake; yeye naye **alitubu/alijutia dhambi zake hadharani bila kumwonea Yesu aibu wakati akiwa hai na Yesu akaiona nia ya ndani ya moyo wake ndipo akampokea**!!***Luk. 23:39-43*** akamwambia leo hii utakua nami Paradiso.
- **(Paradiso) maana yake ni uweponi mwa Mungu au tuite ni Mbinguni;** yaani tangu Yesu Kristo alipokufa pale msalabani, na kushuka chini kuzimu anakoishi ibilisi na wafuasi wake; **aliwahamisha kabisa watakatifu walio kuwa nao wakifa wanakwenda chini na wanakuwa wanawaona waliokufa katika dhambi na kuzungumza nao, kasoro tu wametengwa na shimo kubwa ili wasitembeleane!!** ***Luk. 16:22-26,*** akawahamishia **Paradiso.** ***Math.27:50-54.*** **Iko tofauti kubwa sana mbele za Mungu kwa mtu anayefia dhambini na mtu aliyetubu dhambi zake.** ***Ufun 14:13. Aliyekufa akiwa ameokoka (ametubu) anapokelewa peponi na kupumzika!!***

- **Ndiyo sababu Mtume Paulo alisisitiza sana ndugu zake Wayahudi watubu/ wajutie dhambi zao wakati wakiwa hai na baada ya toba waanze kuishi maisha yanayoendana na toba yao na watende pia matendo yanayopatana na kutubu kwao maana kwa neema yeye alichukuliwa hadi Mbingu ya tatu na huko hakuwakuta waalimu wake waliomfundisha torati na baadaye wakafa na wala**

**hakuwakuta makuhani wake ambao walimpinga Yesu na baadaye kumshitaki na kisha kumsulubisha kwa sababu ya kutoshika sabato yao na kuponya wagonjwa siku hiyo.*Mdo. 26:19-23, (2 Kor.12:1-10)***

La muhimu sana kufahamu ni hili kamba kujutia dhambi (toba) kuna faida kwa mtu aliye hai maana binadamu yeyote anapokufa, anakabiliana na hukumu ya Mungu kama

***Dan.12:1-4*** alivyoonyeshwa na kama Mtume Paulo anavyosema kwa mkazo sana katika kitabu cha Waebrania kwamba watu wote wamewekwa kufa mara moja tu na baada ya kufa "**HUKUMU" *Ebr.9:23-28.***

- **Hatima ya mtu ya baadaye anaitengeneza mwenyewe sasa hata kama ni ya maisha ya hapa duniani; na kama ambavyo haiwezekani mtu kutengeneza hatima ya maisha yake ya hapa Ulimwenguni baada ya kufa kwake; vivyo hivyo haiwezekani kabisa kutengeneza hatima yako ya baadaye huko mbinguni baada ya kufa hata iwe ni kwa kufanyiwa ibada na kutolewa sadaka na ndugu zako au viongozi wako wa dini!! Haiwezekani!! *Luka. 16:23-26***
- Pamoja na toba na kulia sana na majuto makubwa sana ya tajiri huyu ambaye hata jina lake halijulikani; bado toba yake ilikataliwa na Yesu kwa kuwa hana upendeleo, hawezi kamwe kumkatalia ndugu yetu huyu tajiri aliyejuta na kulia sana kuhusu maisha yake ya dhambi halafu aje akusamehe wewe leo ambaye hutaki kutubu kabisa dhambi zako na kuziacha ukivizia kutubu dakika ya mwisho au kuombewa na ndugu zako au na viongozi wako wa dini baada ya kufa.
- **Hadi hapo dhambi itakapokuumiza moyoni mwako na kutambua madhara yake ndipo utakapoijutia na kuiacha kabisa kuanzia leo; lakini kama unaona faida ya dhambi hiyo kamwe hutaiacha hadi itakapokuangamiza kabisa kama ilivyokuwa kwa AKANI- *Yosh. 7:1, 16-26***
- Ni vema sana kila mwana wa Mungu akajutia dhambi zake zote leo hasa zile dhambi za siri ambazo hapana mtu anayezifahamu lakini mbele za Mungu zinasimama na ndizo zitakazofanya **uaibike** milele na milele siku ile.***Dan. 12:1-3. Amina***.

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***